Bibli Inakusema juu ya . . .

Δ

Imetafisiriwa na Philip M. Rimbani,

Imechukuliwawa toka masomo ya

WILLIE WHITE

SOMO LA 01 – Biblia Inakusema juu ya MUNGU

"Kwa maana mtu amwendeaye ni lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao (Ebr. 11:6)

Kuwa mkristo inaanza na Mungu. "kwa maana mtu amwendeaye ni lazima aamini kwamba yeye ndiye."yawezekanaje kiumbe kuhoji uwepo wa muumba?

Ushahidi wa uwepo wa nafsi hai ya Mungu una pita ufahamu zote *Mtunga zaburi* analia. "Mpumbavu amesema moyoni mwake Hakuna Mungu (Zaburi 14:1). Mpumbavu anafafanuliwa kama "mtu asiye na ufahamu, na asiyetumia akili katika maamuzi yake". Ni jambo la busara kumwamini Mungu

Swali kuhusu kuwepo kwa Mungu ni la ki-msingi kwa kila mmoja. Waungwana wengi huuliza, "Nitajuaje kuwa kuna nafsi hai iitwayo Mungu?" kuhusu Mungu zingatia ushahidi ufuatao

1. <u>USHAHIDI WA KIASILI</u>

Watu wa kila mahali kwa nyakati zote wameshikilia namna mbalimbali za imani na nguvu na shauku ya kuabudu. Mungu alituumba na kiu isiyo na ukomo kwa ajili yake. Kwa mantiki hiyo, binadamu kwa hali aliyoumbiwa hutumia uwezo na nguvu ambao ni zaidi ya ufahamu wake, na hii ndiyo inayotudhihirishia kuwa iko nguvu ya ajabu mahali Fulani. "ni muhimu mno kutokuwa kweli"

2. <u>USHAHIDI WA CHANZO NA TUKIO</u>

Wanasayansi wetu zamani walituambia kuwa "kila tukio lina sababu yake maalum." Chanzo kikubwa pekee kilichosababisha kuwepo kwa ulimwengu, mtu, kanisa, Biblia, maombi kujibiwa, kubadilika watu, na uhakika wa moyo wa mwamini ni Yehova Mungu! " yeye aliyevitengeneza vitu vyote ni Mungu" (Ebr. 3:4)

3. <u>USHAHIDI WA KIMAFUNUO</u>

Kama angekuwepo Muumba, basi angejifunua kwa viumbe wake. Mungu Yehova amejifunua kwa mwenyewe kwa mwanadamu kwa njia ya Biblia, kitabu pekee kinachomnena Mungu kwa ufasaha na kupitia mwanawe Yesu ambaye alikiri, "Aliyeniona mimi amemuona Baba." (Yh 14:9). Kwa kupitia mwana tuliweza kumfahamu Baba. "mada huelezea uwepo, historia huelezea hatma, falisafa dhumuni, lakini Yesu tu humfunua Baba

Kama tunavyosoma tabia za Yehova Mungu, kumbuka kuwa yote yanayoonyesha yeye ni nini, yanaonyesha yeye ndiye

1. Tunajuaje kuwa Mungu ndiye?
   a: (Zaburi 42:1, _____
   _____
   b: (Zaburi 19:1;Rum 1:20) _____
   _____
   c: (Rum 15:4, Ebr 1:1, 2; John 14:1)_____
   _____
2. Ni nani basi huyo asemaye hakuna Mungu?
3. Mungu anafananaje?
   a: (Yoh. 4:24)
   b: (1Yoh. 1:5)
   c: (1Yoh 4:8)
   d: (Ebr. 12:29)

Namna gani tunaweza kumfahamu Mungu? (Yoh. 14:9)

Kumbuka Yesu alisema kwamba "*Aliyeniona mimi amemuona Baba."* Soma mistari ifuatayo na kasha jibu kwa kujaza nafasi zilizo wazi

a. (Mt. 9:36; Yoh. 11:35) _____

b. (Yoh. 8:1-11) _____
c. (Yoh. 2:13-17) _____
d. (Yoh. 13:1) _____

6. Andiko linatukumbusha kuwa Mungu “ni **mtunuku** wa wote wamtafutao kwa bidii.” Ni tunu gani apatayo mtu kwa kumtafuta Mungu? (Yer. 29:13) _____
_____
7. Je Mungu yuko mbali nasi? **(Mdo. 17:27,28)** _____
_____

8. Ni jambo gani ambalo Mungu ametufanyia
a: (Mw 1:1) _____
b: (Yoh. 3:16) _____
c: (Zab. 103:12) _____
d: (Mdo. 5:32) _____
e: (Yer. 33:3) _____

9. Je, Mungu anamhitaji mwanadamu? (2Pt 3:9)

SOMO LA 02 – Biblia inakusema juu ya KRISTO

Matthew 16:16 "**THOU ART THE CHRIST, THE SON OF THE LIVING GOD**"

Kama karne 19½ zilizopita hivi, ng'ambo nchi ya mbali kilizaliwa kitoto ambacho kilipewa jina YESU. Halijalishi watu wanachoamini juu yake, lakini walao wanajua kuwa kulikuwa na mtu aitwaye Yesu. Kalenda inatuthibitishia kuwa si habari zake si hadithi ni kweli; mistari ya tarehe ya dunia inabadilikia kwenye hori la Bethlehem. Swali si kwamba "je Yesu aliishi?" bali "Yeye ni nani?" "Wewe je, unamfikiriaje Kristo?" kila kitu chenye maana na umilele vinatoa jibu lako. Je ipi ni mizani ya uthibitisho, na sababu ya sisi kuamini kuwa Yesu ni mwana wa Mungu mtakatifu?

1. KUZALIWA KWAKE KULIKUWA KWA MWANA WA MUNGU (Math. 1:18)
Kuzaliwa kwa **ajabu** kwa mtoto **Bethelehem** kamwe hakujawahi kutiliwa mashaka. Alikuwa mwana wa Mungu aliyezaliwa kwenye **hori** la kulishia wanyama.

2. MAISHA YAKE YALIKUWA NI MAISHA YA MWANA WA MUNGU
Yeye alikuwa na nguvu juu ya mfumo wa asili, nguvu dhidi ya magonjwa, na maradhi, nguvu dhidi ya mauti. Alivunja kila aina ya mazishi aliyowahi kuhudhuria! Uhakika na ukweli wake unabainika vema licha ya "maisha yake yeye mwenyewe kuwa muujiza, yangekuwa muujiza kama asingefanya miujiza wakati wa huduma yake.maisha yake ya kutotenda dhambi, kutenda miujiza kunathihirisha uungu wake

3. KIFO CHAKE KILIKUWA KIFO CHA MWANA WA MUNGU
Maisha yake hayakuondolewa , yalitolewa! Kwa maana alitabiri kifo chake na kikiendea kwa unyoofu msalabani. Alilia kiasi kwamba hata mashuhuda walioshuhudia walilia wakisema. "ama kwa hakika huyu alikuwa mtoto wa Mungu". Na hata mwizi aliyekuwa anakufa alimtajakama mfalme.

4. UFUFUO WA ULIKUWA WA USHINDI WA KIMUNGU
Hakuna dhana ya uhakika katika matukio ya kihistoria kama kufufuka kwa Yesu Kristo, kwani "alithibitishwa kama mwana wa Mungu …. Kwa kufufuka kwake toka kwa wafu" (Rum. 1:4)

5. UWEZO WAKE SASA NI UWEZO WA MWANA WA MUNGU
Hata baada ya karne 19 bado anatenda kazi katika ulimwengu. Imo nguvu ibadilishayo wenye dhambi na kuwafanya watakatifu. "hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya ; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya" (2Krt. 5:17)

Tutahusianishwaje na Yesu wa Nazareti kama hatumkiri kama alivyomkiri Petro, "wewe ni Kristo mwana wa Mungu aliye juu?"

1. Manabii walimsema Kristo kuwa ni nani?
   a. Musa (kumb. 18:15) _____
   b. Mika. (Mik. 5:2) _____
   c. Isaya (Isay. 53:4-6) _____

2. Mungu mwenyewe alimnena Yesu kama nani?
   a. (Mt. 3:17; 17:5) _____
      _____
   b. (Mt. 1:21; Luk. 2:11) _____

_____

3. Wanafunzi wa Yesu walimnena Kristo kuwa ni nani?
   a. Petro (Math. 16:16) _____
   b. Filipo (Yoh. 1:45) _____
   c. Yohana. (Yoh. 1:1) _____
   d. Thomaso (Yoh. 20:28)
   e. Yuda Iskariote (Mt. 27:4)

4. Watu wengine walimnena Kristo kuwa ni nani?
   a. Nikodemu (Yoh. 3:2) _____
   b. Maofisa (Yoh. 7:46) _____
   c. Mhanga mmoja. (Yoh. 9:25) _____
   d. Pilato (Luk. 23:4) _____
   e. Mke wa Pilato (Mt. 27:19) _____
   f. Akida (Mt. 27:54) _____

5. Yesu mwenyewe alijinena kuwa ni nani?
   a. (Yoh. 4:25,26) _____
   b. (Yoh. 10:30) _____
   c. (Mk. 14:61,62) _____
      (Mt.9: 6) _____
      (Mt. 12:6) _____
      (Mt. 12:8) _____
      (Mt.12: 41) _____
      (Mt. 12:42) _____
   f. (Mt. 25:31,32) _____

6. Ni uthibitisho gani mkubwa wa uungu wa Yesu Kristo? (Rum. 1:4) _____
7. Ni matokeo gani ya kukataa kuamini uungu wa Yesu? _____
8. ni thawabu gani apatayo mtu anapoamini katika uungu wa Yesu? _____
   _____

SOMO LA 03 – Biblia inkusema juu ya ROHO MTAKATIFU

"**ROHO MTAKATIFU; AMBAYE MUNGU AMEWAPA WALE WOTE WAMWAMINIO**" MDO. 5:32

"MDO. 5:32. Sisi ni mashahidi wa mambo haya ndiyo maana Mungu amewapa wote wamwaminio Roho Mtakatifu."

Dhana moja ya muhimu sana na ambayo halieleweki na pia kupuuzwa katika Biblia ni **habari za Roho Mtakatifu** "Roho wa Mungu" kama tafsiri nyingine za Biblia (toleo la kimarekani) na mengineo mengi yanavyomwiita. Hebu basi tujifunze hili somo kwa makini na kwa maombi

1. ROHO MTAKATIFU NI NINI?

Roho mtakatifu ni nafsi hai kamili ya Mungu na sio kitu kisichokuwepo katika utendaji wake! Katika Biblia **kiwakilish**i cha jina na jinsia ya '**me'** inatumika kila mara atajwapo.Roho Mtakatifu anachukua tabia za mtu wa kawaida kabisa. Anasemekana kufikiria, hunia, kupenda na kuhuzunishwa. Ana majina mengi kama Roho wa Mungu, Roho wa Kristo, Roho wa utakatifu, Roho wa kweli, Roho wa upendo, nk. Mungu Baba, Mungu mwana, Mungu Roho mtakatifu huunda neon liitwalo "MUNGU."

Constitute

2. ROHO MTAKATIFU HUFANYA NINI?

Mambo yote afanyayo Mungu hapa duniani huyafanya kwa kupitia "Roho wake"Roho mtakatifu amekuwa akitenda kazi katika uumbaji, ufunuo na ukombozi. (Mw. 1:2; 2Ptr.1: 21; Yoh. 16:8).

3. ROHO MTAKATIFU HUTOLEWAJE?

a. Roho mtakatifu alitolewa kwa Yesu bila kipimo wakati wa kubatizwa kwake, akimwezesha kuwa na nguvu zisizo na mipaka (Mt. 3:16).
b. Roho Mtakatifu alitolewa nakumwagwa juu ya mitume kwa kusudi takatifu la Mungu (wayahudi) (Mdo.2) na kwa nyumba nzima ya Kornelio (Mmataifa) (Mdo.10). huu ubatizo wa Roho uliiwezesha nyumba nzima ya Kornelio kunena kwa lugha mpya, ushahidi tosha dhidi ya wayahudi kuonyesha kuwa mataifa pia wanakubalika mbele ya Mungu nakuwapa mitume nguvu na uwezo wa kutenda miujiza na kugawa karama za Roho kwa wengine (Mdo.2:43; 8:18).
c. Roho Mtakatifu alitolewa kwa viongozi waliochaguliwa tu katika kanisa la mwanzo kwa kuwekewa mikono na mitume (Mdo.8: 18) ambayo matokeo yake ni karama na vipawa vinavyoa ambatana na matendo ya miujiza
d. Roho mtakatifu ni ahadi ya kila mkristo ili mradi tu anamtii kristo (mdo. 2:38). Huu uwepo uishio ndani ambao humtia nguvu, kufariji na kumwongoza mtoto wa Mungu, na kumwezesha kuzaa matunda ya Roho (Gal. 5:22,23). Hata wewe pia, hii nguvu inapatikana kwako; usisite kudai kile ambacho Mungu amekuahidia (Lk. 11:13).

1. ni majina gani matatu yanayo nafsi za Mungu (Mt. 28:19)? _____
2. Orodhesha tabia tatu za Roho Mtakatifu _____
   a. Example (Rum. 8:27) Roho mtakatifu hufikiri
   b. (Rum. 15:30) _____
   c. (1Kor. 12:11) Roho mtakatifu hufikiri _____
   d. (Ef. 4:30) _____
   e. (Mt. 12:31,32)_____

f. (Mdo. 7:51) _____

3. Roho mtakatifu alikuwa na kazi gani wakati wa agano la kale?
   a. (Mw. 1:2) _____
   b. (Kt. 31:1 – 5) _____
   c. (Amu. 3:10; 6:34) _____
   d. (1Sam. 10:10; 19:20; 1Ptr. 1:10, 11) _____

4. Ni lini Yesu alimpokea Nguvu za Roho mtakatifu? (Mt. 3:16) _____
   _____

5. Yesu alipokea nguvu za Roho mtakatifu kiasi gani? (Yoh. 3:34) _____
   _____

6. Roho mtakatifu alifanya nini kwa mitume?
   a. (Yoh. 14:16,17) _____
   b. (Lk. 12:12) _____
   c. (Yoh. 16:13) _____
   d. (Mdo. 1:5) _____

7. Ni makundi yapi mawili ya watu waliobatizwa kwa Roho mtakatifu? (Mdo. 1:26- 2:4; 10:44 – 47;11:15) _____

8. Kuna aina ngapi za karama muhimu za miujiza zitolewazo? (Mdo. 8:18)
   _____

9. Ni namna gani tunavyompokea Roho mtakatifu Leo? (Mdo. 2:38; 5:32) _____
   _____

10. Mambo gani ambayo Roho mtakatifu anawafanyia wakristo?
    a. (Efe. 1:13) _____
    b. (Rum. 8:26) _____
       _____
    c. (Rum. 8:16) _____
       _____
    d. (Gal. 5:16,18) _____
       _____
    e. (Efe. 3:16) _____
    f. (Rum. 5:5) _____
       _____
    g. (Rum. 8:11) _____

11. Tunda la Roho ni nini katika maisha ya Mkristo? (Gal. 5:22,23)
    a. _____ f. _____
    b. _____ g. _____
    c. _____ h. _____
    d. _____ i. _____
    e. _____

LESSON – 04 Biblia Inakusema juu ya BIBLIA

"WATU WA MUNGU WALINENA KAMA WATU WALIOONGOZWA NA ROHO MTAKATIFU" 2PET. 1:21

Biblia ni kitabu cha Mungu cha ajabu. Ni maktaba ya vitabu sitini na sita, kilichoandikwa kwa lugha tatu tofauti, na watu arobaini (40) ambao waliishi katika mataifa si chini ya sita, kikiandikwa kwa muda wa zaidi ya miaka 1600. pamoja na mtawanyiko huu wote bado tunakuta umoja wa ajabu. Ni namna gani itaelezeka?. Biblia yenyewe inadai kuwa Mungu ndiye aliyeiandika (Mhariri). "Maandiko yote yametolewa kwa uvuvio wa Mungu" (2Tim. 3:16). Biblia katika kurasa zake imenena Mara 2600 kuwa imetoka kwa Mungu. Kupitia mikono ya watu (wanadamu) waliovuviwa. Je ni **kweli** ya Mungu au **Uongo** wa mwanadamu? Tunajuaje basi kuwa Biblia ni neno la Mungu lililovuviwa?

1. BIBLIA INASEMA YALE AMBAYO HAKUNA KITABU KINGINE KITACHOWEZA KUYASEMA

Biblia inafika mbali sana nyuma kuliko kitabu kingine chochote kilichoandikwa na binadamu: "Hapo mwanzo Mungu" (Mw. 1:1). Biblia inafika mbali sana mbele kuliko kitabu kingine chochote kilichoandikwa na binadamu. "Milele na Milele (Ufu. 20:10). Historia imeandikwa kabla haijatokea! Kama miaka 1400 hivi kabla hata ya kuzalliwa kwa Yesu; kuzaliwa kwake, maisha yake na kifo chake vilielezewa (tabiriwa) kiundani kwa namna ya ajabu. Unabii uliotimia ni ushahidi tosha kwa uvuvio wa Biblia.

Biblia imejaa mawazo ambayo ni mawazo yatakayotoka kwa Mungu pekee. Wazo la Mungu, wazo la uumbaji, wazo la mwanadamu, wazo la umilele ni makubwa mno kuaminika kuwa mwanzo wake ni kwenye ufahamu ya binadamu. Biblia inatuambia kwanini tuko hapa duniani, tumetoka wapi na tunakwenda wapi.

2. BIBLIA INAVUMILIA KILE AMBACHO HAKUNA KITABU KINGINE KINACHOWEZA KUVUMILIA

Dhoruba za karne zimeupiga huu mwamba wa zamani, lakini Biblia imebaki kuwa imara. Vipimo mbalimbali na matemo yamekuja na kupita Biblia imebaki imara. "Ee Bwana, neon lako lasimama imara mbinguni hata milele" (Zab. 119:89). Ni kweli "kwa neon la Mungu lenye uzima lidumulo hata milele." (1Pet. 1:23)"

3. BIBLIA INAFANYA YALE AMBAYO HAKUNA KITABU KINGINE KINACHOWEZA KUFANYA

Biblia inafundisha watu wasio na adili kuwa waadilifu. some, zungumuza na maneno ya kitabu hiki popote pale kwa wakati wowote ule katika historia yake utakuwa umejiongezea maarifa na maadili mema. Biblia ina nguvu ya kufunua dhambi, kubadilisha maisha na kuumba imani katika mioyo ya watu. "Kwa maana siionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye" (Rum. 1:16)

1. ni kitabu gani kikubwa kuliko vyoye duniani? _____
2. toa majina matatu ya kiroho yenye maana sawa na Biblia
   a. (Ef. 6:17; 1Pet. 1:23) _____
   b. (Mt. 21:42; Yoh. 5:39; Mdo. 17:11) _____
   c. (Ebr. 5:12; Mdo. 7:38) _____
3. kuna vitabu vingapi katika Biblia? _____
4. Biblia imegawanyika katika mafungu makuu mawili ni yape hayo? _____

a. _____
b. _____

5. ni agano gani katika Biblia ambalo ni mwongozo kwa wakristo? _____
6. nani aliyeandika Biblia? (2Tim. 3:16; 2Pet. 1:21) _____
7. kamusi inatoa tafsiri gani sahihi ya neno Uvuvio? _____
   _____
8. Nini tafsiri sahihi katika kamusi ya neno "**unabii**" toka kwenye? _____
   _____
9. Nini thamani ya kusoma **Biblia**? _____
   a. (2Tim. 2:15) _____
   b. (2Tim. 3:15) _____
   c. (Yoh. 8:32) _____
10. Vitabu vingine ambavyo ni muhimu kwa mwandamu katika kumyajua mapenzi Mungu? (2Tim. 3:16, 17)
11. Je, ni kweli kwamba (2Tim. 3:16, 17) ina maana sawa na asemavyo Mtume Paulo?
    a. _____
    b. _____
    c. _____
    d. _____
    e. _____
12. Ni nini matokeo ya kupunguza au kuongeza chochote katika neno la Mungu?(Ufu. 22:18, 19)
    _____
    _____
13. Taja sababu zilizokufanya wewe kuamini kuwa Biblia ni neno la Mungu lenye uvuvio.
    _____
    _____
    _____
14. Kama Biblia ni neno la Mungu kwetu, nini Mtazamo wetu tunapoisoma?
    _____
    _____
    _____
    _____

SOMO LA – 05 Biblia inakusema juu ya KANISA

"NA JUU YA MWAMBA HUU NITALIJENGA KANISA LANGU." – MATHAYO 16:18

Ilikuwa ni wakati petro alipovuviwa akamkiri Yesu ndipo Yesu naye akanena hayo maneno. "Na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu na milango ya kuzimu haitalishinda." Alitimiza ahadi yake siku ya Pentekoste baada ya kusulubiwa na kufufuka alituma Roho mtakatifu kwa wanafunzi (wafuasi) wake kuwatia nguvu katika kuliimarisha kanisa. (Mdo. 2:1 – 41).

Kwa karne 19 kanisa lake limekuwepo duniani. Wengi wamekuwa wakilikejeli kanisa, wengine kulipinga, wengine kulipuuza; na bado wapo waliopata amani na furaha ya ajabu kuwa ndani ya kanisa. Tunaweza kuliamini kanisa kwa sababu zifuatazo.

1. TUNAWEZA KULIAMINI KANISA KWA SABABU YA <u>CHANZO CHAKE</u>

Kanisa ni mpango/fikra kamili ya Mungu (1Kor. 1:1, 2), ulionunuliwa na Kristo mwana wa Mungu (Mdo. 20:28), na hatimaye kuanzishwa duniani na Roho wa Mungu mwenyewe (Mdo. 2)

2. **TUNAWEZA KULIAMINI KANISA KWA SABABU YA MFUMO WAKE WA KIUONGOZI**

Kiongozi/kichwa cha kanisa ni kitakatifu. (Kol. 1:18), kielelezo kamili cha uongozi(Ef. 4:11,12), mpango mtakatifu wa kiserikali/kiutawala. (Mdo. 6:1 – 6). Kkwa sababu ya huu mpango mtakatifu wa kiungozi "hata milango ya kuzimu kamwe shinda kanisa"

3. **TUNAWEZA KULIAMINI KANISA KWA SABABU YA UMOJA WAKE**

Kanisa ni mjumuisho wa watu waliookoka. Sio kwamba ni wakamilifu, bali ni watu waliosikia wito wa Mungu na kujinyenyekeza, katika amri zake na "wakikazana kufikia ukamilifu."

4. **TUNAWEZA KULIAMINI KANISA KWA SABABU YA UTIMILIFU WAKE**

Kanisa limekusanya na kuhifadhi maandiko matakatifu. Kanisa limewezesha watu kumwabudu Mungu. Kanisa siku zote limebeba ujumbe ambao unafundisha na unaelimisha ulimwengu, kubadilisha, kuokoa na kutoa makusudi na maana ya maisha.

5. **TUNAWEZA KULIAMINI KANISA KWA SABABU YA UMILELE WAKE**

Malango ya kuzimu haijawahi kamwe kulishinda kanisa. Ukristo wa kweli hauwezi kuharibiwa, kwa maana ndani yake hakuna kinachoweza kuharibika.
KANISA NI MWILI WA KRISTO – HAUTAONA UHARIBIFU;
KANISA NI NYUMBA YA KRISTO – KAMWE HAIWEZI UHARIBIFU;
KANISA NI MKE WA KRISTO – HAWEZI KUACHWA;
Tafadhali tupende na kulijali kanisa, tukikumbuka kuwa hata "Kristo pia alilipenda na akajitoa kwa ajili yake." (Ef. 5:25)

1. Kanisa ni nini?
   a. (Ef. 1:22, 23) _____
   b. (Ef. 5:24, 25) _____
   c. (1Tim. 3:15) _____
2. Nani mwanzilishi wa kanisa? (1Kor. 1:1, 2; (Ef. 1:3,4) _____
   _____
3. Kanisa lilinunuliwa kwa gharama gani? (Mdo. 20:28) _____
   _____
4. Kanisa lilianzishwa lini? (Mdo. 2:1, 41) _____
   _____

5. Ni wapi kanisa lilianzia? (Isa. 3:3; Mdo.1: 4; 2:5) _____
_____
6. Ni nguvu gani kanisa lishushiwa ili kulipa uhai? (Mdo. 2:1-4) _____
_____
_____
7. Watu walifanya nini ili kuwa washirika katika katika kanisa la mwanzo? _____
   a. _____
   b. _____
   c. _____
   d. _____
8. Ni nani aliyeongeza waumini katika kanisa la kwanzo? (Mdo. 2:47) _____
9. Ni njia gani nne walizotumia wakristo wa kwanza kuendelea kiimani? (Mdo. 2:42)
   a. _____
   b. _____
   c. _____
   d. _____
10. Ni nani kichwa cha Kanisa? (Mt. 28:18;Ef. 1:22,23) _____
11. Msingi wa kanisa ni nini? (1Kor. 3:11; Ef. 2:19, 20)
_____
_____
12. Ni majengo mangapi yanasimamishwa juu ya msingi mmoja? _____
13. Kanisa la mwanzo lilikutania wapi? (Mdo. 2:46;Rum.16: 5; 1Kor. 16:19) _____
_____
14. Mungu alilipa Kanisa majina gani?
   a. (1Kor. 1:2)_____
   b. (Ebr. 12:23)_____
   c. (1Kor. 12:27)_____
   d. (Rum.16: 16) _____
   e. (1Tim. 3:15) _____
   f. (Rum.16: 4) _____
   g. (Mdo. 8:1, 3; 15:3,4; 18:22) _____
15. Neno “Kanisa” lina maana gani kwako? _____
_____
_____
16. Nini hatima ya “**Kanisa**”? (The.4: 16,17) _____
_____
_____
17. nini tafsiri sahihi ya neno “**Kanisa**” toka kwenye kamusi? _____
_____
_____
_____
18. Nini tafsiri sahihi ya neno “**ushirika**” toka kwenye kamusi
_____
_____
_____
_____

SOMO LA – 06 Biblia Inakusema juu ya DHAMBI

"WOTE WAMETENDA DHAMBI NA KUPUNGUKIWA NA UTUKUFU WA MUNGU" – RUM. 3:23

"Wajinga husahabikia dhambi na wanafalsafa hutoa tafsiri yake", Lakini kama kuna dhana iliyojificha ni dhana ya dhambi. Tunaijua dhambi kwa namna mbali mbali kama uchunguzi, uzoevu, ushuhuda wa neno la Mungu. Dira yetu, Biblia inatumbia chanzo chake, madhara yake na Tiba yake.

1. **CHANZO CHA DHAMBI**
   sura ya tatu ya kitabu cha mwanzo inatumbia chanzo cha dhambi hapa duniani. Yehova Mungu alimpa mwanadamu kula kila aina ya matunda katika miti ya bustani ya Edeni, isipokuwa matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya na akawatahadharisha kutokula mti wa memana mabaya, "kwa maana siku mtakayo kula kwa hakika mtakufa" (Mw. 2:17). Nyoka akajamjia Eva kwa swali, "Ati hivi ndivyo Mungu alivyosema?," na kukanusha kauli ya Mungu kwa kusema "Kwa hakika hamtakufa."mwanamke akakata tunda alilokatazwa akala na kumpa mumewe naye akala. Dhambi iliingia duniani kwa njia ya kusikia, kuamini na kutii uongo.

2. **MADHARA YA DHAMBI**
   Dhambi ni kitendo cha kumwasi Mungu, na kamwe hakitaepuka adhabu. Kama madhara ya dhambi, macho ya Adam na Eva yalifunguliwa; na wakajijua wa uchi wakajificha machoni pa Yehova. Siku zote dhambi inamtenga mtu na Mungu. Kwa sababu ya kutokutii huku, Mungu akaamuru laana juu ya nyoka, mwanamke, mwanamume na dunia. (Mw. 3:14 – 19). Na madhara zaidi ya dhambi mwandamu akafukuzwa katika bustani ya Edeni na asije akagusa mti wa uzima. "kwa maana **mshahara wa dhambai ni mauti**" (Rum. 6:23)

3. **TIBA YA DHAMBI**
   Picha ingekuwa ya giza tororo kama tungekuwa tunajua tu chanzo na madhara ya dhambi. Mungu wetu atupendaye sana ametoa namna ya kusamehewa dhambi. Katika sura ileile tuliyoona chanzo cha dhambi Mungu aliahidi kumtoa yule taliyemponda nyoka kichwa (Mw. 3:15). Karne nyingi baadaye Yohana mbatizaji alimtambulisha Yesu wa Nazareth akisema "Tazama Mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Yoh. 1:29). Dhambi husamehewa tu pale ambapo mtu anakubali, kumtii Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi. Dhambi iliingia duniani kwa njia ya kusikia, kuamini na kutii uongo, dhambi inasamehewa kwa njia ya Dhambi iliingia duniani kwa njia ya kusikia, kuamini na kutii uongo kweli.

1. Dhambi ni nini?
   a. (1Yoh. 3:4)_____
   b. (1Yoh. 5:17)_____
   c. (Yak. 4:17))_____
2. Nini madhara ya dhambi kama ilivyoainishwa kwenye kitabu cha Mwanzo?
   a. (Mstari wa 7)_____
      _____
   b. (Mstari wa 8)_____
      _____
   c. (Mstari wa 14, 15)_____
      _____
   d. (Mstari wa 16)_____
      _____
   e. (Mstari wa 17, 19)_____
      _____

f. (Mstari wa 22, 24)_____
_____

3. Ni adhabu gani ya mwisho kwa dhambi?_____
   a. (Rum. 6:23; 5:12; Yk. 1:15) _____
   b. (Mt. 25:41) _____
4. Ni wangapi wametenda dhambi? (Rum. 3:23; Isa. 53:6) _____
5. Je, Mungu hutujaribu kutenda dhambi? (Yk. 1:13) _____
6. Ni nani basi atujaribuye kutenda dhambi? _____
   a. (Mt. 4:1 – 3) _____
   b. (Yk. 1:14) _____
7. Je, wakristo wanatenda dhambi? (Rum. 7:22 – 25; 1Yoh. 1:10)_____
   _____
8. Je, ni lazima kushindwa mara tunapojaribiwa na dhambi? _____
   _____
9. Je, kuna ahadi yeyote aliyoitoa Mungu juu ya kusamehe dhambi zetu? (Isa. 1:18;Yer. 31:34; Mt. 6:14) _____
10. Nani awezaye kusamehe dhambi? (Mt. 1:21; Yoh. 1:29) _____
11. Yesu anawezaje kusamehe dhambi?
    a. (Ebr. 9:24) _____
    b. (2Kor. 5:21) _____
12. Tunawezaje kuishinda dhambi? (Ufu. 12:11) _____
    a. _____
    b. _____
    c. _____
13. nini tafsiri ya maneno yafuatayo toka kwenye kamusi?
    a. Dhambi_____
    b. Jaribu _____
    c. Maovu _____
    _____

SOMO LA - 07 Biblia Inakusema juu ya WOKOVU

"MWISHO WA IMANI YAKO NA WOKOVU WA NAFSI YAKO." 1PET. 1:19

Malaika wa Bwana alipomtokea Yusufu katika ndoto kumtia moyo ili amchukue kama mke wake, ilishatangazwa kabla kuwa Mariamu atamzaa mwana na jina lake ataitwa Yesu, "kwa maana atawaokoa watu wake na dhambi zao" (Mt. 1:21). Kama kuna ukweli wenye kubariki katika neno la Mungu ni kukombolewa kwa nafsi zenu." Biblia imetufunulia kweli zifuatazo kuhusu **Wokovu**.

1. WOTE WANAHITAJI KUOKOLEWA:

a. wote wanahitaji kuokolewa kutokana na mateso ya dhambi. "Wote wametenda dhambi nakupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Rum. 3:23). Kwa sababu wote wametenda dhambi, basi wote wanahitaji msamaha wa dhambi zao

b. wote wanahitaji kuokolewa toka katika nguvu ya dhambi. Kwa sababu wote tumetenda dhambi, basi wote tunahitaji kuokolewa kutoka katika nguvu ya dhambi maishani mwetu. Tunahitaji nguvu ya kushinda dhambi.

c. Wote wanahitaji kuokolewa kutoka katika **ADHABU** ya dhambi. "kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti" (Rum. 6:23). Watu wote wanahitaji mwokozi wa kuwaokoa kutaka katika adhabu ya dhambi.

2. WOTE WANAWEZA KUOKOLEWA:

Mwaliko wa Yesu Mwokozi wa ulimwengu ni "njooni kwangu ninyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo ya dhambi nami nitawapumzisha. (Mt. 11:28). "kama mtu akisikia sauti yangu na kufungulia, nitaingia" (Ufu. 3:20). Mwaliko wake wa neema ni kwa "**WOTE"**, kwa "**AWAYEYOTE"** na kwa "**KILA MTU**."

3. IPO NJIA MOJA TU:

Mtume Petro aliweka wazi kwa Kuhani Mkuu (Mdo. 4:12) "wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote; kwa maana hapan jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo kuokolewa kwalo." Njia ya wokovu ni Yesu Kristo mwana wa Mungu, ambaye alinena katika Yoh. 14:6, "Mimi ndimi njia, kweli na uzima:mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi. Yesu pekee anaweza kumwokoa mtu na mateso, nguvu na adhabu ya dhambi.
Huu ni ujumbe wa ajabu wa neno la Mungu kwamba: "atawaokoa watu wake na dhambi zao."

1. Kwa nini mtoto wa Mariamu aliitwa Yesu? (Mt. 1:21) _____
   _____
2. Ni watu wanahitaji kuokolewa? (Rum. 5:12) _____
3. Wangapi wanaweza kuokolewa?
   a. (Mt. 11:28) _____
   b. (Ufu. 3:20) _____
   c. (Yoh. 3:16) _____
4. ni hatua zipi tatu anazopaswa mtu kupitia ili kuokoka? (Zingatia maandiko hapo juu)
   a. _____
   b. _____
   c. _____
5. ni nani pekee awezaye kuokoa? (Mdo. 4:10 – 12) _____
   _____
6. Yesu anawezaje kutuokoa toka katika mateso ya Dhambi? (2Kor. 5:21)_____
   _____
   _____

7. Yesu anawezaje kutuokoa toka katika nguvu ya Dhambi? (Flp. 4:13)_____
_____
_____

8. Yesu anawezaje kutuokoa toka katika adhabu ya Dhambi? (Ebr. 7:25; 1Yoh.2: 1)_____
_____
_____

9. sadaka ya wanyama iliyotolewa agano la kale inaweza kumpa mtu ondoleo la dhambi? ____
(Ebr. 10:4) _____
_____

10. Je tunaweza kuokolewa kwa matendo yetu mema? (Mt. 7: 22,23) _____
_____

11. haki yetu yaweza kutuokoka? (Tit. 3:5; Isa. 64:6) _____
_____

12. Ni nini kituokoacho?
    a. (Tit. 3:5) _____
    b. (Efe.2:8) _____
    c. (Efe.1:5 - 7; 1Pet. 1:18,19) _____
    d. (1Pet. 3:20,21) _____

13. Sehemu ya Mungu ni ipi katika wokovu wa mwanadamu?
    a. (Yoh. 3:16) _____
    b. (Yoh. 14:16; 16:18) _____
    _____

14. Sehemu ya mwanadamu ni ipi katika wokovu wake yeye mwenyewe?
    a. (Mdo. 2:40)_____
    b. (Mdo. 16:31)_____
    c. (Mdo. 3:19) _____
    d. (Rum. 10:9,10) _____
    e. (Mk. 16:16) _____
    f. (Mdo. 2:42; Ufu. 2:10) _____

15. nini tafsiri sahihi ya maneno yafuatayo toka katika kamusi?
    a. Wokovu _____
    _____
    b. Msamaha _____
    _____
    c. Komboa _____
    _____

SOMO LA – 08 Biblia Inakusema juu ya IMANI

"LAKINI PASIPO IMANI HAIWEZEKANI KUMPENDEZA;" EBR. 11:6

"Yanipasa nifanye nini ili niweze kuokoka?" swali la ajabu kabisa lililoulizwa katika jela ya filipi (Mdo. 16. jawabu lilikuwa rahisi kama nini kama lilivyotolewa na Paulo na Sila katika mstari wa 31: "mwamini Yesu Kristo nawe utaokoka." Soma Matendo 16:16 – 34 utakuta kuwa imani ndiyo iokoayo.

1. **IMANI YETU IWEKWE PAMOJA NA MWANA WA MUNGU: "MWAMINI BWANA YESU"**
   Kwa kigiriki ***kiunganishi*** "en" kina maana ya "juu ya" au "ndani ya" au "ndani kwenye". Kuna tofauti kubwa kati ya kumwamini mtu, na kuamini ndani ya mtu. Tunapoamini mtu tunakuwa na ujasiri na tunaonyesha nia ya kuheshimu nafasi aliyonayo tu.

2. **IMANI YETU NI KWA BWANA: "AMINI KATIKA BWANA"**
   Neno "BWANA" lina maana ya "HABABI," "MTAWALA," au "MKUU." Tunapomkubali Yesu kama Bwana, tunamkubali kama, **Mtawala** wetu na tunatakiwa kutenda aliyotuamuru.

3. **IMANI YETU NI KWA YESU: "MWAMINI BWANA YESU."**
   Jina Yesu lina maana ya "MWOKOZI" (Mt. 1:21). Tunapomkubali kama Yesu tunakubali matakwa yake yote, uwezo wake wa kutuokoa toka dhambini,

4. IMANI YETU KWA KRISTO: "MWAMINI BWANA YESU KRISTO"
   Lazima tumkubali Yesu kama Kristo na "**mpakwa mafuta**" wa Mungu (Yoh.20:30, 31). Manabii, Makuhani na Wafalme *walisimikwa* kwa kupakwa mafuta matakatifu; kwa maana hiyo tunaposema kuwa Yesu ni Kristo, tunamkubali kama nabii, kuhani na mfalme wetu.

5. **IMANI YETU NI LAZIMA <u>IJIONYESHE</u> KIUTII**:
   Mkuu wa gereza la Filipi aliosha majeraha ya akina Paul an Sila, akidhihirisha **toba** yake na akabatizwa yeye na nyumba yake yote. Imani iokoayo ni imani ituongozayo katika kutii amri za Kristo. Ni kiasi gani cha imani kiwezacho kuokoa? Ni kiasi tu cha kutusababisha kumkubali Kristo.
   Mkuu wa gereza "alishangilia, kumwamini Mungu yeye na nyumba yake." Kuna furaha ya ajabu katika moyo wa mwanadamu pale anapomwamini Mungu na kuamini neno lake.

1. nini tafsiri sahihi ya neno IMANI toka kwenye kamusi? _____
   _____
2. nini tafsiri sahihi ya neno IMANI toka kwenye Biblia? (Ebr. 11:1) _____
   _____
3. Je, tunawezakumpendeza Mungu pasipo Imani? (Ebr. 11:6) _____
   _____
4. Chanzo cha imani ni nini? (Rum. 10:17) _____
   _____
5. nini hatima ya imani?
   a. (Mdo. 15:9) _____
   b. (Mdo. 26:18) _____
   c. (Rum. 5:1) _____
   d. (Gal. 3:26) _____

e. (Efe. 2:8) _____
f. (Yoh. 3:16) _____
g. (Mt. 21:22) _____
h. (Mk. 9:23) _____

6. mwisho wa imani yetu ni nini? (1Pet. 1:9) _____
_____

7. Ni mambo gani yalifanywa kwa “imani” na wafuatao?
a. Abeli (Ebr. 11:4) _____
b. Henoko (Ebr. 11:5) _____
c. Nuhu (Ebr. 11:7) _____
d. Sara (Ebr. 11:11) _____
e. Ibrahim (Ebr. 11:8 – 1) _____
_____
f. Musa (Ebr. 11:23 – 28) _____
_____

8. Ni namna gani tunaweza kuonyesha imani yetu? (Yk. 2:20) _____
_____

9. yesu alituambia tuamini nini (Yoh. 14:1) _____
_____

10. nini tuamini toka kwa Yesu? (Mt. 16:16) _____
_____

11. Nini maana ya neno “Bwana”? _____
_____

12. Nini maana ya neno “Kristo”? _____
_____

13. Ni makundi ya aina ngapi za watu waliopakwa mafuta nyakati za Biblia? _____
a. (1Fal. 19:16) _____
b. (Law. 3:4) _____
c. (2Sam. 5:3) _____

14. Ni mambo yapi mawili **yaliyomstaajabisha** Yesu?
a. (Mt. 8:10) _____
b. (Mk.6: 6) _____

15. Ni jambo gani ambalo Yesu alilikemea kwa masisitizo? (Mt. 6:30; 8:26) _____
_____

16. Nini madhara ya kukataa kumwamini Yesu? (Mk. 16:16; Yoh. 8:24) _____
_____
_____
_____

17. watu wa kwanza waliomwamini Yesu aliuliza swali gani? (Mdo. 2:37,38) _____
_____
_____

SOMO LA 09 – Biblia Inakusema juu ya TOBA

"TUBUNI BASI, MREJEE, ILI DHAMBI ZENU ZIFUTWE" – Mdo 3:19

mojawapo ya dhana ambayo haizoeleki au isiyoeleweka kwa wengi katika Biblia ni **Toba**. Wengi huifanya toba kama sherehe, na wengine hudhani wanapotoa machozi na maombi ya kulalama basi huwa ndio wameshatubu;wengine wanaifikiria toba kama sikitiko baada ya kutenda dhambi au kutenda kosa la jinai! Basi tuangalie Biblia inasemaje juu ya hatua hii ya muhimu kwa mtu yeyote anapotaka kuwa Mkristo.

1. **MAANAYA TOBA KIBIBLIA**
   Neno la kigriki katika Matendo 3:19 n.k na ambalo limetafisiriwa kwa kiingereza "**toba**" lina maana ya sawa na "**kubadili fikra**"

2. **BIBLIA INATUAMBIA NINI KUFANYA TOBA YA KWELI**
   wema wa Mungu (Rum. 2:4), imani katika Yesu Kristo na nguvu ya dhamba katika maisha yetu (Mdo. 2:37, 38) na huzuni ya Kimungu juu ya dhambi (2Kor. 7:9, 10) siku zote zinavuta mabadiliko ya kweli ya fikra dhidi ya dhambi.
3. **BIBLIA INATUAMBIA NINI KINAFUATA BAADA YA TOBA**
   a. utii unaambatana na toba ya kweli (Mdo. 2:41)
   b. msamaha unafuata baada ya toba na utii (Mdo. 3:19).
   c. mwenendo uliobadilika unafuata baada ya toba. Neno linatuagiza "**kutubu**; na kubadishwa (kugeuka)." Tunafanya toba ya kweli. Tunakua na shauku ya kupatana na wale tuliowakosea, kama alivyofanya Zakayo mtoza ushuru. (Lk. 19:8).

4. **BIBLIA INATUAMBIA NI NANI ANAYE STAHILI KUTUBU**
   "Anawaamuru watu wa kila mahali kutubu" (Mdo. 17:30). Sawa sawa na "wote wametenda dhambi" (Rum. 3:23), wote wanastahili kutubu. Bwana hapendi hata mmoja apotee, bali kwamba wafikilie toba (2Pet. 3:9). Ni jambo la zuri namna gani kwamba kila mmoja wetu afikie toba, kwa maana "**pasipo**" kutuba kwa hakika wote tutaangamia." (Lk. 13:3)

1. Nini tafsiri sahihi ya neno **toba** toka kwenye kamusi? _____
   _____
2. Nini maana ya neno **"toba"** katika Biblia kama lilivyotafsiriwa toka lugha ya Kigiriki? _____
   _____
3. Ni nani anayehitaji toba? (Mdo.17:30) _____
   _____
4. kwa nini wanadamu wote wanahitaji kutubu? (Rum. 3:23) _____
   _____
5. kwa nini tunatakiwa kutubu kwa mujibu wa (Mdo. 17:30,31)? _____
   _____
6. Yesu alisema alikuja ulimwenguni kwa sababu gani? (Lk. 5:32) _____
   _____
7. Nini kinachotuongoza kwenye toba? _____
   a. (Rum. 2:4) _____
   b. (2Kor. 7:9, 10) _____
8. Tunatubu dhambi zetu kwa nani? (Mdo. 20:21) _____

9. Roho mtakatifu hutusaidiaje kutubu? (Yoh. 16:8) _____
_____
10. Mungu aliwaambia watu waliotubu kufanya nini? (Mdo. 2:38; 22:16) _____
_____
_____
11. Ni mambo gani mawili waliyoahidiwa watu waliotubu na kubatizwa? (Mdo. 2:38) _____
    a. _____
    b. _____
12. Nini kinachofuata baada ya **toba**? (Mdo. 3:19)
    a. _____
    b. _____
13. Ni toba ya namna gani alivyoonyesha mwana mpotevu? (Lk. 15:20) _____
_____
_____
14. Nini kinachotokea mbinguni mwenye dhambi mmoja anapotubu duniani? (Lk. 15:7) _____
_____
15. Nini tunachopaswa kufanya baada ya kutubu na kumgeukia Mungu? (Mdo.26:20) _____
_____
_____
16. Je, wakristo wanahitaji kutubu? (Mdo. 8:18 – 22; Ufu. 2:5) _____
17. Je, Mungu anajali toba? (2Pet. 3:9) _____
18. Nini hatima yetu tusipotubu? (Lk. 13:3) _____
_____
19. Ni vema toba kuhubiriwa kanisani? (Lk. 24:47) _____
20. Nini tafsiri sahihi ya neno **kurejelea** toka kwenye kamusi? _____
_____
_____
21. toa maelezo yako mwenyewe kwa nini unaamini kila mtu anastahili kutubu _____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____

SOMO LA – 10 Biblia Inakusema juu ya MAUNGAMO

"**KWA ULIMI MTU HUKIRI HATA KUPATA WOKOVU**." Warumi 10:10

Ilikuwa ni wakati Petro kwa imani yake alipomkiri Yesu, "Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa langu" (Mt. 16:18). Paulo aliwaandikia wakristo wa Rumi "kwa ulimi mtu hukiri hata kupata Wokovu." (Rum. 10:10) "Maungamo mazuri" (1Tim. 6:12) ni muhimi kwani ni hatua katika kuokoka kwetu!

1. **MAUNGAMO MAZURI NI KWA NJIA YA ULIMI (RUM. 10:10)**

Mara tu baada ya kuamini kwa mioyo yetu yote kwamba Yesu ni Kristo mwana wa Mungu aliye hai, tunaamini hivyo nakukiri kwa njia ya vinywa.

2. **MAUNGAMO MAZURI YANAMKUBALI YESU KAMA BWANA.**

"**Yesu kama Bwana**." Namna hii ya kumkubali ni ya kuinua ukuu na ubawana Wake: ni bwana wangu – mimi ni mtumwa wake; anaponena mimi natii. Wengi wanamkubali Yesu kama **Mwokozi** na sio wengi wanaomkubali kama **Bwana**.

3. **MAUNGAMO MAZURI LAZIMA YATOKE KATIKA MOYO UNAOAMINI**

"amini kwa moyo wako kuwa Mungu alimfufua toka kwa wafu" (Rum. 10:9). Na hili ndilo jiwe la kufungia: imani katika ufufuo wa Kristo. Ufufuo wa Yesu ni jambo la Uhakika, kwani watu walimwamini kama mwana wa Mungu baada ya kufufuka. (Rum. 1:4).

4. **MAUNGAMO MAZURI YANAMKUBALI YESU KAMA KRISTO, MWANA WA MUNGU.**

Haya ni maungamo aliyoungama Petro, na ukiri ambao kanisa limejengwa juu yake. Tunapokiri na kuamini kuwa Yesu ni Kristo, tunamkubali kama mpakwa mafuta wa Mungu: Nabii wetu, Kuhani na Mfalme, Mesiya wa Agano la kale na Mwana wa Mungu aliyehai..

5. MAUNGAMO MAZURI NI YALE YANAFANYWA HADHARANI.

Ni mwana wa Mungu mwenyewe aliyeahidi "Yeyote atakayenikiri mbele ya wanadamu, nami nitamkiri mbele ya Baba yangu wa mbinguni" (Mt. 10:32). Yesu alijaribiwa hadharani, aliteswa hadharani na alikufa hadharani kwa ajili yetu. Je, kipo cha zaidi anachodai kwetu anapotuambia kumkiri mbele za watu?

Je, unaamini moyoni mwako kuwa Yesu ni Kristo, mwana wa Mungu na kwamba Mungu alimfufua toka kwa wafu? Utamkiri mbele za watu? "sasa ni siku ya wokovu"

1. Paulo aliyaitaje maungamo ya imani yetu? (1Tim. 6:12) _____
   _____
2. kwa nini maungamo mazuri ya muhimu? (Rum. 10:9,10) _____
   _____
   _____
3. Yesu alisema atafanya nini kwa wale watakaomkiri mbele za wanadamu? (Mt. 10:32) _____
   _____
4. Yesu alisema atafanya nini kwa wale watakaomkana mbele za wanadamu? (Mt. 10:33) _____

_____
_____

5. Nathanaeli alito maungamo ya namna gani? (Yoh. 49) _____
_____
6. Petro alito maungamo ya namna gani? (16:16) _____
_____
7. Yule Towashi wa kushi alito maungamo ya namna gani? (Mdo. 8:37) _____
_____
8. Ni neno gani la muhimu lililoongezwa katika (Rum. 10:9) ambalo halikutajwa katika maungamo matatu hapo juu? _____
9. tunamaanisha nini tunapokiri kuwa Yesu ni Bwana? _____
_____
10. Nini tunachotakiwa kufanya kama kweli Yesu ni Bwana? _____
_____
11. Tuamini nini tunapofanya Maungamo mazuri? _____
_____
12. Ni ushahidi gani unaotufanya kuamini juu ya ufufuo wa Yesu?
    a. (Yoh. 20:3 – 8) _____
    b. (Mt. 28:2 – 6) _____
    c. (Lk. 24:8 – 10) _____
    d. (Mt. 28:11 – 15) _____
    e. (1Kor. 15:5 – 8) _____
        1. _____
        2. _____
        3. _____
        4. _____
        5. _____
        6. _____
    f. (Flp. 3:10; 2Kor. 5:17) _____
13. Matokeo yangekuwaje kama Kristo hakufufuka? (1Kor. 15:14 – 19) _____
_____
    a. _____
    b. _____
    c. _____
    d. _____
    e. _____
14. Ni kwa nini baadhi ya wanadamu hawapendi kuafanya maungamo ya mazur? (1Kor. 15:14 – 19)
_____
_____
15. Unafikiri hatimaye wanadamu wote watamkiri Kristo? (Rum. 14:11) _____
_____
16. Kwa nini ni tunahitajika kumkiri Yesu mbele za watu?_____
_____
_____
_____

SOMO LA 11 – Biblia Inakusema juu ya UBATIZO

"AAMINIYE NA KUBATIZWA ATAOKOKA." MK. 16:16

ubatizo wa kikristo ni kitendo cha utii na upendo wa ahadi takatifu. Jambo la kwanza kabisa alilolifanya Yesu katika huduma yake ilikuwa ni kubatizwa hadharani katika mto Yordani.(Mt. 3:13-17). Agizo la mwisho la bwana Yesu kwa wanafunzi wake lilikuwa ni "basi enendeni ulimwenguni mwote mkawafanye mataifa kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la mwana na la Roho Mtakatifu." (Mt. 28:19). Siku kanisa lilipozaliwa Petro alielekeza akiwaagiza washirika, "Tubuni na kubatizwa kila mmoja wenu kwa jina la Bwana Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" (Mdo. 2:28)

1. **NANI ANAYESTAHILI KUBATIZWA?**

Ubatizo ni kwa wale walioisikia injili (Mdo18:8), wanaoiamini injili (Mk. 16:16), waliotubu (Mdo. 2:28), na wale waliofanyika kuwa wafuasi au wanafunzi (Mt. 28:19). Hao tu ndio watahiniwa wa kiroho wa ubatizo.

2. **TUNATAKIWA KUBATIZWA NAMNA GANI?**

Tutakujaona katika sehemu ya kijitabu nini kinachotakiwa katika kuendesha ubatizo wa ki-Biblia. Kwa KI-GIRIKI neno (BAPTIDZO) lina maana ya kuzamisha, kupiga mbizi, ingiza ndani ya. Kuzamisha ndani ya maji ndio neno pekee linalotoa maana halisi ya ubatizo ki-Biblia. Ubatizo ni kuzikwa kwa mwilio wa muumini mgonjwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi

3. **KWA NINI TUNATAKIWA KUBATIZWA?**

Tunatakiwa kubatizwa ili kusamehewa dhambi zetu (Mdo. 22:16), "kumvaa Kristo" (Gal. 3:27), kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu (Mdo. 2:38), na kuongezwa katika kanisa la Kristo (Mdo. 2:41).

Petro alitamka kuwa ubatizo unaokoa (1Pet. 3:21). Kufuatisha utaratibu tu haiokoi, maji hayaokoi, kinachookoa ni utii. Ubatizo ni kitendo cha kupenda utii na agizo kamili takatifu; Yesu alisema, "mtu akinipenda na kuzishika amri zangu" (Yoh. 14:15). Je, unampenda Yesu? Kama ndio, basi utajitahidi siku zote kutii amri zake.

1. Nini maana ya neno Ubatizo? _____
   _____
2. Nani aliyeonyesha mfano wa ubatizo wetu? (Mt. 3:13) _____
   _____
3. Yesu alibatiziwa wapi? (Mt. 3:13) _____
4. Ni sababu gani ya msingi Yesu alitoa ya kutamani kubatizwa? (Mt. 3:15) _____
   _____
   _____
   _____
5. Nini kilitokea mara baada ya kubatizwa kwa Yesu? (Mt. 3:16,17) _____
   _____
   _____
6. Nani anayestahili ubatizo?
   a. (Mdo. 18:8) _____
   b. (Mk. 16:16) _____
   c. (Mdo. 2:38) _____
   d. (Mt. 28:19) _____
7. kulingana na maandiko hapo juu, mtoto anaweza kubatizwa? _____

8. Kuna aina (maana) ngapi za ubatizo?(Efe. 5:4) _____
9. nini kinachotakiwa katika kuendesha ubatizo wa Kikristo? Pata mwongozo wa namna za batizo kutoka katika mistari ifuatayo
   a. (Mdo. 8: 36) _____
   b. (Yoh. 3:23) _____
   c. (Mt. 3:13) _____
   d. (Mdo. 8:38) _____
   e. (Mdo. 8:39) _____
   f. (Yoh. 3:5) _____
   g. (Kol. 2:12) _____
   h. (Rum. 6:4) _____
   i. (Ebr. 10:22) _____
10. kulimgana na maandiko hapo juu ni vema sisi kubatizwa kwa kunyunyiziwa maji au kumwagiwa maji? _____
11. ni kweli zipi kuu tatu za injili zinazotubidikutimiza tunapo batizwa? _____
    _____
    _____
    _____
12. Yesu aliwaahidi nini wale wote ambao wangeliamini na kubatizwa? (Mark 16:16) _____
    _____
    _____
13. Ni mambo yapi mawili ambayo Petro aliwaahidi wote ambao wangelitubu na kubatizwa?
    a. _____
    b. _____
14. ni sababu gani ambayo mtume Paulo alitoa juu ya ubatizo? (Gal. 3:27) _____
    _____
15. Ni wakati gani katika mpango wa Mungu ambapo mwenye dhambi anaiitia damu ya Yesu? (Rum. 6:3) _____
    _____
16. Petro alisema ubatizo unakazi gani kwetu? (1Pet. 3:21) _____
    _____
17. nini matokeo ya kukataa kutenda yale tunayotakiwa kutenda? (Yk. 4:17) _____
    _____
    _____
18. ni sababu gani ingekuwa ya msingi kwetu katika kubatizwa? (Yoh. 14:15) _____
19. nini tunachotakiwa kufanya baada ya kubatizwa? _____
    a. (Rum. 6:4) _____
    b. (Mdo. 2:42) _____

SOMO LA 12 – Biblia Inakusema juu ya KUZALIWA UPYA

"LAZIMA UZALIWE MARA YA PILI" (YOH. 3:7)

Mtu mmoja mkuu wa mafarisayo jina lake Nikodemu mtawala wa wayahudi alimjia Yesu usiku na mzigo moyoni mwake. Ni kwa kiongozi huyu wa dini Yesu alimwambia "Ni lazima uzaliwe mara ya pili" hebu na tujifunze kitabu Yohana 3: 1- 8 tuone jinsi Yesu alipofundisha maana ya kuzaliwa upya.

1. YESU ALIFUNDISHA KUWA KUZALIWA UPYA NI LAZIMA KUZALIWATENA.
   "Ni lazima uzaliwe mara ya pili" (Yoh. 3:7,3). Kabila ya kiumbe hai chochote kuzaliwa mara ya pili ni lazima kuwe na kufa na kuzikwa. Lazima tufe kwa dhambi (Kol. 3:3) na tuzikwe katika maji ya ubatizo wa Kikristo ili tufufuliwe kwa upya wa uzima. (Rum. 6:1 – 4).

2. YESU ALIFUNDISHA KUWA KUZALIWA UPYA NI MUHIMU ZAIDI
   kuzaliwa upya ni kwa maana zaidi katika ufalme wa Mungu.: Yesu akasema "mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuuona ufame wa Mungu." Kuzaliwa upya ni kwa muhimu sana kwa ajili ya kutuwezesha kuuingia ufalme wa Mungu: "mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuuingia ufalme wa Mungu" (Yoh. 3:5).

3. YESU ALIFUNDISHA KUWA KUZALIWA UPYA KUNATIMIA PALE MTU ANAPOZALIWA KWA MAJI NA ROHO
   Yesu aliposema kuwa ni lazima mtu azaliwe kwa maji, alikuwa anazungumzia hatua ya kuuingia ufalme. Alikuwa ana maanisha kuzaliwa kwa maji alipokuwa anazungumza katika (Mk. 16:16), "aaminiye na kubatizwa ataokoka." Petro alikuwa anazungumzia kuzaliwa kwa maji siku ya Pentekoste alipoita umati wa watu kuja kutubu na kubatizwa na kupata ondoleo la dhambi zao. (Mdo. 2:38).

   Lakini kuzaliwa kwa maji tu ni sehemu ya tu ya kuzaliwa upya; lazima pia kuwe na kuzaliwa kwa Roho. Ni nguvu za Roho Mtakatifu zinazomfanya muumini mtiifu awe kiumbe kipya ndani ya Kristo. (2Kor. 5:17). Roho Mtakatifu alikuja ulimwenguni kwa ajili ya kuwashuhudia wanadamu kwa habari ya dhambi. (Yoh. 16:7,8). Roho Mtakatifu ametupatia neno la Mungu, ambalo limetupa maisha mapya. (1Pet. 1:23). Tumeahidiwa Roho Mtakatifu tangia tunapozaliwa mara ya pili. (Mdo. 2:38,39). Sio kuzaliwa kwa maji wala kwa Roho tunakotakiwa kupuuza, bali kwa kuzitii amri za Bwana wetu atupendaye na mamlaka yake ya ajabu tumefanyika viumbe wapya katika Kristo Yesu.

1. Nikodemu ni nani? (Yoh. 3:1) _____
   _____
2. Yesu alisema ni lazima tufanyeje ili kuuona ufalme wa Mungu? (Yoh. 3:3) _____
   _____
3. Ni nini tunachotakiwa kufanya kabla ya kuzaliwa upya?
   a. (Gal. 2:20; Kol. 3:3) _____
   b. (Rum. 6:1 – 4) _____
4. Je inatosha tu kubadilika nje? (Mt. 23:25) _____
   _____
5. Yesu alisema ni lazima tufanye nini ili kuuingia ufalme wa Mungu? (Yoh. 3:5)
   _____
6. Watu elfu tatu walifanya nini siku ya Pentekoste ili kuuingia ufalme wa Mungu? (Mdo. 2:37-41) _____

_____
_____
_____

7. Yule towashi mkushi alifanya nini ili kuuingia ufalme wa Mungu? (Mdo. 8:35-39) _____
_____
8. Lidya alifanya nini ili kuuingia ufalme wa Mungu (Mdo. 16:14,15) _____
_____
9. Mkuu wa gereza la filipi alifanya nini ili kuuingia ufalme wa Mungu? (Mdo. 16: 29-34) _____
_____
_____
10. Wakorintho walifanya nini ili kuuingia ufalme wa Mungu? (Mdo. 18:8) _____
_____
_____
11. Sauli wa Tarso alifanya nini ili kuuingia ufalme wa Mungu? (Mdo. 22:6-16) _____
_____
_____
12. Tunamvaaje Kristo katika maisha yetu? (Gal. 3:26,27) _____
_____
13. Kama mtu akiwa ndani ya Kristo anakuwa mtu wa namna gani? (2Kor. 5:17) _____
14. Roho Mtakatifu anatusaidiaje kufanyika viumbe wapya?
    a. (Yoh. 16:7,8) _____
    _____
    b. (2Pet1: 21; 1Pet.1: 23) _____
    _____
    c. (Mdo.2: 38) _____
    _____
    d. (Rum. 8:13) _____
    _____
    e. (Rum. 8:14) _____
    _____
    f. (Gal. 5:22,23) _____
    _____
15. Sasa fikiria masomo yote 12 uliyopitia huko nyuma, kasha andika kwa maneno yako wewe mwenyewe kwa nini unafikiri ni vema kwa kila mtu kumkubali Kristo na kufanyika kiumbe kipya ndani yake.

_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____

HITIMISHO

Kama umepitia masomo haya yote bila kukata shauri na kutii amri za Bwana Yesu kikamilifu na hujawahi kumuungamia Yesu kama Bwana, hujawahi kutubu dhambi zako, na hujawahi kuzamishwa, utafanya huo uwamuzi sasa?